KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 11, Issue 4

22nd RAJAB 1432

24th June, 2011

YALIYOMO

UHARAMU WA NYIMBO 1 - 4

UHARAMU WA NYIMBO [Prt 2]

Mtayarishi: Sheikh Sa'd ad-Deen ibn Muhammad al-Kibbi

Ibn Abi Shaybah (رحمه الله) alihadithia yakwamba mtu mmoja alivunja mandolin (chombo fulani cha mziki kilichofungwa nyuzi). ya mtu mwengine na yule aliye vunjiwa akapeleka mashtaka kwa Shurayh (رحمه الله) (hakimu mashuhuri aliyekuwa na akihukmu kwa uadilifu). Lakini Shurayh hakumpa malipo yoyote- yaani hakumfanya mwenye kuvunja alipe thamani ya mandolin hiyo, kwa sababu ilikuwa ni haraam na haina thamani. (al-Musannaf, 5/395).

Al-Baghawi (رحمه الله) alisema katika fatwa kuwa: ni haraam kuuza ala zote za mziki kama tamboor na zumari na kila kinachohusiana na mziki. kisha akasema ikiwa sura (picha) zitafutwa na vyombo vya mziki vikabadilishwa (kufanywa viti vingine) basi yaruhusiwa kuuza vipande vyake ikiwa ni fedha, chuma, mbao au vyenginevyo. (Sharhu al -Sunnah 8/28)

KILICHOKUBALIWA KWA USAWA

Kinachokubaliwa katika yaliyotangulia hapo juu ni *Daff* (twari)- lilisilo na vitasa au vikengele na mfano wake, linapotumiwa na wanawake siku za 'Eid na harusi. Hii imeashiriwa kwa hadeeth swaheeh.

Ibn Taymiyyah alisema: "Lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliruhusu sampuli fulani za ala za mziki katika harusi na mfano wake, na akaruhusu wanawake kupiga matwari kwenye maharusi na katika tamasha nyingine. Lakini waume katika zama zake hawakupiga matwari wala makofi. Imehadithiwa kwenye as-Swaheeh yakwamba alisema: "Kupiga makofi ni kwa wanawake na tasbeeh (*Subhaan Allah*) ni kwa wanaume." Na akawalaani wanawake wenye kujifananisha na wanaume na wanaume wenye kujifananisha na wanawake. Kwa sababu kuimba na kupiga matwari ni vitu vifanywavyo na wanawake, as-Salaf walikuwa wakimwita mtu yoyote mwenye kufanya hivyo kuwa ni mukhannath (khanithi) – na walikuwa wakiwaita waimbaji wakiume makhanithi - na ni wangapi waliopo leo? Na yajulikana vyema yakwamba as-Salaf us-Swaalih walisema hivyo.

Kwenye mshipa kama huo ni hadeeth ya 'Aaisha (رضي الله عنها) wakati babake

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

قافلة الرحمة للحج والعمرة Al-Rahma `Umrah & Hajj

Agencies1432 Hijri / 2011 C.E

Assalaamu `Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah Safari yetu ya mwaka huu 1432 Hijri/2011 ya kupeleka watu `Umrah katika mwezi wa Ramadhaan, kumi la mwisho. Na vilevile katika `Ibaadah ya Hijjah.

Mipangilio ya Safari ya `Umrah (Mwezi wa Ramadhaan) ni kama ifuatayo:

• Kuondoka ni tarehe 17 ya mwezi wa Ramadhaan*Kurudi ni baada ya `Eid Insha Allaah

• Safari itaanzia Nairobi – Jeddah

• Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli na Usafiri) ni $1500 U.S

• Siku tatu tutakuwa Madinah na Siku kumi za mwisho tutakuwa Makkah mpaka `Eid.

• Safari ya Kurudi Jeddah – Nairobi. Itakuwa baada ya `Eid

Twapenda kuwahimiza wale wale wenye niya ya kwenda na sisi waharakishe kuleta Passport zao na picha Nne kwa ajili ya kufanya maandalizi. Sababu ni kwamba Viza zitafungwa kabla ya mweizi wa Ramadhaan kuanza.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa njia zifuatazo:

• Tutumie e-mail katika info@qssea.net au

• Simu nambari +254 723471820 (Abu Bilaal Athman Na'man)

• Simu nambari +254 721473181 (Abu Farida Muhammad Basawad)

• Simu nambari +254 700365253 (Muhammad Abdillaah)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

(رضي الله عنه) alipoingia nyumbani kwake wakati wa 'Eid, na palikuwa na wasichana wawili pamoja nae ambao waliokuwa wakiimba beti za *Answaar* walizozisema katika siku ya Bu'aath - na kila mwenye busara atajua wanayoyasema watu kuhusu vita. Abu Bakr (رضي الله عنه) akasema: "Ala za mziki za Shaytaan ndani ya nyumba ya Mtume wa Allaah! Mtume (صلى الله عليه وسلم)! Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwageukia na kuwapa mgongo akauelekea ukuta - kwahiyo, baadhi ya wanazuoni walisema yakwamba Abu Bakr (رضي الله عنه) hakuweza kumkemea yoyote mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) lakini alidhania yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakushughulika kwa yaliyokuwa yakijiri. Na Allah ndie Mjuzi zaidi. Yeye [Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: "Achana nao ewe Abu Bakr, hakika kila ummah una 'Eid zao, na hii ni 'Eid yetu,watu Waislamu." Hadeeth hii yaonyesha kuwa haikuwa ni katika tabia za Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba zake kukusanyika ili kusikiza nyimbo. Ndipo Abu Bakr as-Sideeq akaziita "Ala za mziki za shaytaan." Na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akakubali na wala hakuyakata maneno hayo aliposema "Waache, kila ummah una 'Eid zao, na hii ni 'Eid yetu." Hii inaashiriya yakwamba sababu ya kuruhusiwa jambo hili ilikuwa ni sababu ya kuwa ni wakati wa 'Eid. Na ukatazo utaendelea kudumu katika nyakati zisizokuwa ni 'Eid, mbali na ruhusa zilizotolewa kwa harusi katika ahaadeeth nyingine. Shaykh al-Albani ililieleza hili katika kitabu chake chenye thamani *Tahreem Aalaat al-Tarab* (uharamu wa ala za mziki). Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliruhusu wasichana wadogo kuimba siku ya 'Eid, kama ilivyotajwa katika hadeeth: "Ili washirikina wajue kuwa katika dini yetu kuna nafasi ya mapumziko." Hakuna ishara yoyote katika hadeeth kuhusu wasichana wawili ambao Mtume (صلى الله عليه وسلم) alokuwa akiwasikiliza. Maamrisho na makatazo ni yenye kuhusiana na kusikiliza, sio kusikia pekee, kama ilivy katika hali ya kuona, hukmu ni zenye kuhusiana na kuangalia kwa kukusudia na wala si kwa bahati mbaya. Kwahivyo, ni wazi yakwamba hili ni la wanawake peke yao. Imam Abu 'Ubayd (رحمه الله) ilieleza daff kuwa ni "kitu kinachochezwa na wanawake)." (Ghareeb al-Hadeeth, 3/64)

KILICHOKUBALIWA KIMAKOSA

Baadhi yao waruhusu ngoma nyakati za vita na hatimae wanazuoni wa kileo wamesema kuwa mziki wa kijeshi unaruhusiwa, lakini hakuna msingi wa jambo hilo kabisa, kwa hoja kadhaa, ya kwanza miongoni mwayo ni kuruhusu jambo bila ushahidi ulio wazi, mbali na maoni matupu na kudhania kuwa hilo ni jambo zuri, ilhali ni baya . Sababu ya pili ni kwamba wanayotakiwa Waislamu kufanya katika nyakati za vita ni kuelekeza nyoyo zao kwa Mola wao. Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: (kwa maana ya tafsiri): "Wanakuuliza kuhusu mali yaliyotekwa (ngawira), yagaiwe vipi?" Sema: "mali yaliyotekwa ni ya Allaah na Mtume (fuateni watakavyo kugawieni) . Basi muogopeni Mwenyezi Mungu na msuluhisheni mambo baina yenu, na mtiini Allaah na Mtume wake ikiwa nyinyi ni katika munaoamini (kweli)." [al-Anfaal 8: (1)]

Lakini kutumi mziki ni kinyume cha fikra hii ya taqwa, na utawapotoa wao kutokamana na kumkumbuka Allaah (سبحانه وتعالى).

Tatu, kutumia mziki ni mojawapo ya mila za kikafiri, na hairuhusiwi kuwaiga wao, haswa ikiwa ni jambo ambalo Allaah amelikaza kwa ujumla kama mziki. (as-Swaheehah, 1/145).

"Hakuna watu wanaopotea baada ya kuwa wameogoka isipokuwa huanzisha mizozo baina yao wenyewe." (swaheeh)

Wengine wanatumia hadeeth ya mahabashi walipocheza msikiti wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama ushahidi kuwa kuimba yaruhusiwa!

Al-Bukhari aliiweka hadeeth hii katika swaheeh yake mlango uitwao: *Baab al -Hiraab wa'l-Daraq Yawm al-'Eid* (Sura -mikuki na ngao siku ya 'Eid).

An-Nawawi (رحمه الله) alisema: "Hii yaonyesha kuwa yaruhusiwa kucheza na silaha na mifano yake msikitini, na akaweka katika harakati nyingine zilizoambatana na Jihaad. (sharh Muslim).

Lakini kama alivyosema al-Haafidh Ibn Hajar (رحمه الله): "Yoyote anayezungumza kuhusu jambo ambalo si fani yake atakuja na mambo ya vituko kama haya (ya kurusu miziki).

Baadhi yao wanatumia kama ushahidi hadeeth tuliyoizungumza hapo juu kuhusu kuimba kwa wasichana wawili. Lakini tutanukuu aliyoyasema Ibn al-Qayyim (رحمه الله) kwa sababu ni muhimu. "Mimi nashangazwa yakwamba unanukuu kama dalili ya kuruhusu kusikiza nyimbo za hali ya juu hadeeth tuliyoitaja kuhusu wasichana wawili chini ya umri wa kubaleghe walipomuimbia mwanamke mdogo katika siku ya 'Eid baadhi ya beti za mashairi ya kiarabu kuhusu ushujaa katika vita na sifa nyengine tukufu. Wawezaje kulinganisha hili na hilo? Kilicho cha kustaajabisha ni kuwa hadeeth hii ni mojawapo ya ushahidi madhubuti dhidi yao. Msema ukweli mtukufu (Abu Bakr al-Sideeq) aliziita ala za mziki za Shaytaan. Na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaridhia uitaji huo, lakini akatoa nafasi katika hali ya wasichana wawili wale ambao hawajafika umri wakubaleghe na majukumu na maneno ya yule ambae nyimbo zake zisizoweza kumfitini yoyote mwenye kuzisikiliza. Yawezekana hili kutumiwa kama ushahidi kuruhusu unayoyafanya na unayoyajua kuhusu kusikiliza mziki yakiwemo ndani yake mambo mabaya yenye kudhihirika? Subhaan Allaah! Vipi watu wanavyoweza kupotezwa namna hiyo! (madaarij al-Saalikeen, 1/493)

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Ibn al-Jawzi (رحمه الله) alisema: "Aisha (رضي الله عنها) alikuwa mdogo wakati huo; hakuna kilichopokewa kutoka kwake baada ya kufika umri wa mas'ulia (kubaleghe) isipokuwa kulaumu vikali uimbaji. Mtoto wa ndugu yake al-Qassim Ibn Muhammad alilaumu vikali uimbaji na akasema hairuhusiwi kuisikiliza, naye alichukua 'ilmu kutoka kwake [Aishah] (Talbees Iblees, 229).

Al-Haafidh Ibn Hajar (رحمه الله) alisema: "Kundi la ki-sufi wanaitumia hadeeth hii- hadeeth kuwahusu wasichana wawili-kama ushahidi kuwa kuimba yaruhusiwa na yaruhusiwa kuisikiliza, emma itaandamwa na ala au bila ya ala. Rai hii imekosolewa kisawasawa kwa matamshi yaliyo wazi ya 'Aisha katika hadeeth ifuatayo ambapo aliposema, "walikuwa si waimbaji." Alionyesha wazi kuwa hawakuwa ni waimbaji - na yaweza ikaeleweka vibaya kutokana na maneno ya hadeeth yenyewe. Kwahivyo tuikisie kwa yaliyopokewa kwenye matamshi kuhusiana na tukio lenyewe na jinsi lilivyotokea. Ili tupunguze hatari ya kwenda kinyume na misingi, (yaani Hadeeth) na Allaah ajuwa zaidi (Fath al-Baari, 2/442-443).

Na kuna watu wenye ujasiri wa kusema kuwa Maswahaba (رضي الله عنهم) na ma-Taabi'een (رحمهم الله) walisikiza nyimbo na hawakuona ubaya wowote kwa hilo!

Al-Fawzaan (حفظه الله) alisema: "Madai yetu kwao ni kwamba watuonyeshe isnaad zilizo swaheeh zinazowafikia Maswahaba na ma-Tabi'een, kushuhudisha wanayowabandika." Kisha akasema: "Imam Muslim alitaja katika utangulizi wa Swaheeh yake yakwamba 'Abdullah Ibn al-Mubaarak alisema: 'Isnaad ni katika sehemu ya dini. Ingekuwa si kwa isnaad yoyote atakaye angesema atakalo.

Wengine walisema ahaadeeth zinazokataza mziki zina makosa tele. Wala hakuna hadeeth ambayo haikukashifiwa na baadhi ya wanazuoni" Ibn Baaz (رحمه الله) amesema: "Hadeeth zilizopokewa kuhusu uharamu ya mziki hazina makosa tele kama inavyodaiwa. Nyingine zimo katika swaheeh al-Bukhari kitabu ambacho kina uswaheeh mkubwa baada ya Qur'an na nyinginezo ni hasan na nyingine ni dha'eef. Lakini kwa sababu yakuwa ni nyingi, na zina isnaad mbali mbali zakusanya ushahidi mpana kuwa kuimba na ala za mziki ni haraam.

Maimamu wote wakubaliana na uswaheeh wa ahaadeeth zinazokataza kuimba na ala za mziki ila Abu Haamid al-Ghazzaali, lakini al-Ghazzaali hakuwa na 'ilmu ya hadeeth na Ibn Hazm (رحمه الله), lakini al-Albani (رحمه الله) alieleza pale Ibn Hazm alipokosea, na Ibn Hazm alisema mwenyewe ikiwa hadeeth yoyote katika hizo itakuwa ni swaheeh, yeye ataifuata. Lakini sasa wana ushahidi kuwa hadeeth hizo ni swaheeh kwa sababu kuna vitabu vingi vya wanazuoni vinavyoeleza kuwa hadeeth hizi ni swaheeh, lakini wazungusha migongo yao na kuzikataa. Wao ni wapindanifu wakupita mipaka kuliko Ibn Hazm na hawafanani nae kamwe. Kwani wao hawastahiki wala simarejeo ya ki-'ilmu.

Wengine walisema kuwa wanazuoni walikataza kuimba kwa sababu imetajwa pamoja na mkusanyiko ambapo pombe hunywewa na mahali ambapo watu hukesha kwa ajili ya kufanya mabaya.

Al-Shawkaani (رحمه الله) alisema: "Jawabu kwa hili ni kuwa kuyataja hayo kwa pamoja haimaanishi pekee kuwa kilicho haraam ni kile kilicho shikanishwa katika hali hii. Au huenda ikamaanisha kuwa zinaa, kama ilivyotajwa katika ahaadeeth, si haraam mpaka itangamanike na pombe na ala za mziki. Kwa kipimo hicho hicho aya kama ifuatayo: "**Hakika yeye alikuwa hamuamini Allaah Mtukufu. Wala hajihimizi wala hahimizi wenzake kulisha maskini.**" (Al- Haqqah-69: 33-34]. Itamaanisha kuwa si haramu kumkufuru Allaah mpaka kuambatane na kutowahimiza watu kulisha maskini. Ikisemwa kuwa ukatazo wa vitu kama hivyo kimoja baada ya chengine imeshuhudishwa katika hadeeth nyengine. Jawabu kwa hilo nikuwa uharamisho wa ala za mziki vile vile anajulikana katika ushahidi mwengine kama ilivyotajwa hapo juu. (Nayl al-Awtaar, 8/107]

Wengine walisema kuwa "maneno ya upuzi" haimanishi kuimba. Ukosoaji wa hilo umetangulia kutajwa .

Al-Qurtubi (رحمه الله) amesema: "Hii- rai yakwamba yamaanisha kuimba - ndiyo rai iliyo bora iliyosemwa kuhusu aya hii, na Ibn Mas'ood aliapa mara tatu kwa jina la Allaah ambaye asiyekuwa Yeye hapana mola mwengine, kuwa yamaanisha kuimba. Kisha akataja maimamu wengine waliosema kama hayo. Kisha akataja rai nyengine kuhusu jambo hilo. Kisha akasema: "Rai ya kwanza ndiyo iliyo bora kuliko nyengine zote zilizotajwa kuhusu jambo hili, kwa sababu ya hadeeth marfoo', na kwa sababu ya maoni ya maswahaba na ma-Taabi'een. (Tafseer al-Qurtubi)

Ibn al-Qayyim (رحمه الله) alisema baada ya kunukuu tafseer hii: "Al-Haakim Ibn 'Abdullaah amesema katika tafseer ya Kitaab al-Mustadrak: Licha yakwamba mwenye kutafuta 'ilmu hii anajua kuwa tafseer ya swahaba aliyeshuhudia kuteremshwa kwa wahyi ni hadeeth iliyo na isnaad kulingana na mashekehe wawili (al-Bukhaari na Muslim). Mahali pengine katika kitabu chake, alisema: "Kwa rai zetu hadeeth hii ina nguvu sawa kama riwaya iliyo marfoo'. Ingawaje tafseer yao bado ingali chini ya kuzidi kuchunguzwa, bado itakubalika kuliko tafseer ya watakaokuja baada yao, kwa sababu wao ndiwo waliokuwa bora miongoni mwa Ummah huu katika aliowakusudia katika Kitabu Chake. Kiliteremshwa miongoni mwao na wao

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

ndiwo waliokuwa watu wa kwanza kulinganiwa nacho. Waliisikiya tafseer kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa maneno na kwa vitendo. Nao walikuwa ni Waarabu waliofahamu vizuri sana maana halisi ya maneno (ya kiarabu), kwahivyo Waislamu na wajiepushe na kufuata tafseer yoyote kadiri ya uwezo wao. Baadhi yao wanasema yakwamba kuimba ni sampuli ya 'Ibaada ikiwa makusudio ni kumsaidia mtu amtwi'i Allaah!

Ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema: "Ni jambo la kushangaza mno! Ni sampuli gani ya Imani, nuru, busara, uongofu na 'ilmu, inayoweza kupatikana kwa kusikiliza sauti za beti za mziki ndani yake mna mengi yanayosemwa ya haraam, na yanayostahiki hasira na adhabu ya Allaah na Mtume wake? ...Vipi mtu yoyote mwenye chembechembe za busara na imani moyoni mwake aweza kujikurubisha kwa Allaah na kuongeza imani yake kwa kustarehe na kitu kinachochukiwa na Naye na anamchukia mwenye kusema na mwenye kukubali? (Madaarij as-Saalikeen, 1/485)

Ibn Taymiyyah amesema akimzungumzia kuhusu hali ya mtu aliyezoea kusikiliza mziki: "Na utaona kuwa wale waliozoea kusikiliza mziki na ambao kwao wao ni kama chakula na kinywaji hawatakuwa na hamu ya kusikiliza Qur'an au kusikia raha wanapoisikia, na hawahisi katika kusikiliza aya zake kama wanavyohisi wakisikiliza mashairi. Na hakika wanaposikiliza Qur'an hawasikilizi kwa moyo wa kuzingatia na wanazungumza wakati isomwapo, lakini wasikiapo mbinja, na kupiga makofi hupunguza sauti zao na kunyamaza na kusikiliza kwa makini. (Majmoo' al-Fatawa, 11/557)

Wengine wasema kuwa mziki na ala zake zina athari za kulainisha nyoyo za watu na kuleta hali za upole. Hili si kweli, kwa sababu yachemsha matamanio ya kimwili na uovu. Lau ingekuwa yafanya kama wasemavyo, ingelainisha nyoyo za waimbaji na wana mziki na kuzifanya tabia zao zikawa nzuri, lakini karibu wote, kama tujuavyo, wamepotea na wana tabia mbovu.

MWISHO

Labda –kwa wenye busara na wasomi wenye malengo-mukhtasari huu utabainisha yakwamba rai yakuwa mziki unaruhusiwa haina msingi imara. Hakuna rai mbili katika suala hili. Kwahivyo ni lazima tutoe naswaha kwa njia ifaayo, kisha tufuate hatua kwa hatua katika kukataza mziki, Ikiwa tutaweza kufanya hivyo. Tusihadaike kwa umaarufu wa mtu katika zama zetu ambapo watu waliojitolea kwa Uislamu wanakuwa wageni. Yule anayesema kuwa kuimba na ala za mziki zaruhusiwa anaunga mkono kwa urahisi matamanio ya watu wa kileo, kana kwamba halaiki wametoa fatwa na yeye anazikubali tu kirahisi! Suala likichipuka, wataangalia rai za ma-fuqahaa katika suala hili, kisha watachukua rai ilio rahisi, kama wanavyodai. Kisha watatafuta ushahidi, au mjadala wakuokotwa jaani ambao hauna thamani zaidi ya nyama mfu. Mara ngapi watu hawa wameruhusu mambo kwa jina la sharee'ah ambapo hakuna uhisiano wowote na Uislamu!

Jitahidi na ufanye juhudi kuusoma Uislamu wako kutoka kwenye kitabu cha Allaah (سبحانه وتعالى) na Sunnah za Mtume wake (صلى الله عليه وسلم). Usiseme fulani na fulani wamesema, kwani huwezi kujifunza ukweli kutoka kwa watu. Jifunze ukweli kisha wapime watu dhidi ya ukweli huo. Hili litatosheleza kwa yule anayejichunga na matamanio yake na kujisalimisha nafsi yake kwa Mola wake. Twamuomba Allaah ajaalie tuliyoyaandika yawe ni yenye kutibu nyoyo za waumini na aondoshe ushawishi nyoyoni mwa wale waliopigwa na ushawishi wa shaytaan. Twaomba wa'adhi huu umfedheheshe kila anaye kengeuka kutoka kwenye njia wahyi na kuchukua fursa nyepesi, akifikiri kuwa amekuja na kitu ambacho hakikuwahi kupatikana katika kizazi kilichopita, na kumzungumza Allaah bila ya 'ilmu. Walikuwa wakitafuta kuepukana na fisq (uovu) wakamalizikia kufanya bid'ah— Twamuomba Allaah asiwabariki katika hayo. Ingelikuwa bora kwao kufuata njia ya waumini.Na Allah ajuwa zaidi. Twamuomba Allaah amswalie na kumbariki Mtume wake aliyeiweka njia wazi kwa waumini, na kwa maswahaba wake na wale wenye kuwaandama wao kwa wema mpaka siku ya mwisho.

TWAMUOMBA ALLAH ATUONGOZE

NENO LA BUSARA

'Abdullaah Ibn Mas'ood (رضي الله عنه) amesema:

"Kwa hakika Mu'min huona madhambi yake kama kwamba amesimama chini ya Mlima, akikhofia yakwamba hwenda mlima huo ukamuangukia. Na kwa hakika mtu muovu huona madhambi yake kama kwamba ni *Nzi* wanaoruka na kutua juu ya pua yake na huwafanya hivi." Abu Shihaab (mmojawapo wa wapokezi wa hadeeth hii) akasema (alipokuwa akionyesha kitendo alichokuwa akifanya Ibn Mas'ood aliposema *"na huwafanya hivi"*): humfukuza (Yule *Nzi*) kwa kujikung'uta pua yake kwa mkono wake.

Imepokewa na Imaam al-Bukhaari

JIPATIE NAKALA YA KITABU CHA SWALA:

NAMBARI ZA SIMU NI:

0721473181 AU 0727341779

MOMBASA